

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMSHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

**SHULE YA SEKONDARI IMALA  
S.L.P 129  
URAMBO**

.....

Jina la mwanafunzi .....

S.L.P .....

**URAMBO**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA  
SEKONDARI IMALA MWAKA 20.....**

**1.0 UTANGULIZI**

Uongozi wa shule ya sekondari Imala , inayofuraha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kijiungu na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 20..... Uongozi unakupongeza kwa jithada zako na ni matumaini yetu kuwa jithada hizo utaziongeza uwapo shulenii kwetu. Muhula wa masomo utaanza tarehe ..... unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe ..... (ndani ya siku saba), unahimizwa kuzingatia tarehe ya kuripoti shulenii mapema bila kuchelewa kuanza masomo.

**1.1 MAHALI ILIPO SHULE**

Shule ya sekondari Imala ipo umbali wa km 1 kusini mwa barabara ya Kigoma jirani na makaburi ya Kichangani. Na km 3 kutoka Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo.

**2.0 MAMBO YA KUZINGATIA:-**

**2.1 SARE ZA SHULE.**

**Kwa wavulana:-**

1. Unatakiwa ushone suruali mbili zisizobana (modal), zenye rangi ya jani la mgomba, (isiwe jeans au kodrai) kitambaa cha suti kisicho na michirizi yoyote zenye turn up isiyo chini ya nchi 1 saizi 16 na ziwe na malinda. Pia awe na mkanda wa ngozi mweusi. Atakae kiuka nguo yake itakatwa kwa mkasi.

Mashati mawili tetroni meupe yenyeye mikono mifupi, viatu jozi 2 nyeusi visivyo na visigino virefu wala rangi nyingine tofauti na nyeusi wala mchongoko kwa mbele na viwe vyaa kufunga kwa kamba. Soksi jozi mbili nyeusi.

Tai ndogo (nick tie) ya kitambaa cha suruali.

**NB: Suruali za kubana haziruhusiwi kabisa shulenii.**

### **Kwa wasichana**

2. Unatakiwa ushone sketi mbili zenyе rangi ya jani la mgomba, kitambaa cha suti kisicho na michirizi yejote, ziwe na marinda boksi mawili makubwa (moja mbele moja nyuma) na mawili madogo kwa pembeni, zenyе belt ya inchi 2 na sio zaidi. Urefu lazima iguse vifundo vya miguu (yaani soksi zisionekane)

Mashati mawili tetroni meupe yenye mikono mifupi kwa wanaopenda kuvalaa hijab washone nusu kanzu pamojana juba ndefu ambazo ni nyeupe zisizo na mapambo. Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili, visiwe na kisigino kirefu wala rangi nyingine tofauti na vyeusi, na viwe vya kufunga kwa kamba.

Tai ndogo (nick tie) ya kitambaa cha sketi.

Mambo mengine ya kuzingatia kuhusu sare za shule ni

- i) Mishono ya kihuni haitaruhusiwa shulenii, atakaebainika nguo yake itakatwa kwa mkasi .
- ii) Wakati wa baridi mwanafunzi ataruhusiwa kuvalaa sweta rangi ya kijani mkolezo (dark green) ambazo mzazi/mlezi anaweza kununua mwenyewe.
- iii) Viatu vya wazi (bajaji au raba) haviruhusiwi kuvaliwa shulenii
- iv) Mashati/blauzi/ zinazobana na fupi haziruhusiwi kuvaliwa shulenii atakaebainika nguo yake itakatwa kwa mkasi .

**NB:** Hakikika mwanao ana T – shirt rangi ya kijani ya jeshi (mikono mifupi) kwa ajili ya kazi za jioni na nguo za michezo kwa ajili ya shughuli za michezo.

### **2.2 VIFAA VYA MASOMO**

- ❖ Begi la kubeba daftari
- ❖ Daftari kubwa (counter books) 9 kwa ajili ya nukuu za masomo
- ❖ Daftari ndogo 12 kwa ajili ya mazoezi
- ❖ Mkebe wa hisabati (mathematical set)
- ❖ Kalamu za wino na mkaa.
- ❖ Kamusi ya kiingereza (dictionary)

### **2.3 VIFAA VYA USAFI (leta vilivyowekewa alama ya vema (✓)tu)**

- ❖ Fagio la nje moja la kusimama jipya
- ❖ Jembe moja jipya
- ❖ Fyekeo/kwanja moja jipya
- ❖ Ndoo ndogo moja mpya
- ❖ Reki moja mpya
- ❖ Panga moja jipya

## **2.4. SHERIA NA KANUNI ZA MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı yenyе dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenyе jukumu la usimamizi wa uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shulenı. Mambo hayo ni:-

### **A: HESHIMA:**

- (i) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
- (ii) Mwanafunzi anatakiwa awe MFANO mzuri wa HESHIMA NA TABIA popote atakapokuwa.
- (iii) Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu WANAFUNZI WOTE WA SHULE kujiheshimu yeye mwenyewe na kuwaheshimu wanafunzi wenzake.
- (iv) Mwanafunzi anapaswa kusimama na kuwasalimu wakubwa mahali popote anapokutana nao.
- (v) Mwanafunzi AJIHADHARI NA KAULI CHAFU kwa jamii nzima.

### **B: MAHUDHURIO:**

- (i) Mwanafunzi anapaswa kufika shulenı saa 1:00 asubuhi na kuhudhuria paredi saa 1:30 kila siku ya masomo.
- (ii) Mwanafunzi anapaswa kufika shulenı saa 1:00 asubuhi na kuhudhuria vipindi vyote bila kutokatoka nje ya darasa wakati wa masomo pia ni marufuku kupiga kelele au usumbufu wa aina yoyote darasani.
- (iii) Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria na kushiriki kikamilifu katika kazi za mikono kulingana na maagizo ya shule.
- (iv) Mwanafunzi anapaswa kutii kengele ya shule kulingana na utaratibu au ratiba ya shule.
- (v) Mwanafunzi HARUHUSIWI KUTOKA nje ya eneo la shule bila KIBALI CHA MAANDISHI kutoka kwa mwalimu wa zamu au wa darasa.
- (vi) Mawasiliano yote kutoka kwa wazazi/mlezi yanayomuhusu mwanafunzi kama vile msiba/magonjwa n.k yapitie ofisi ya mkuu wa shule.

### **C: NIDHAMU.**

- (i) Mwanafunzi anapaswa kucaa sare ya shule ya Imala sekondari wakati wote akiwa shulenı au sehemu nyingine kama itakavyoelekezwa na viongozi wa shule. Shati ni lazima lichomekewe na viatu vivaliwe pamoja na soksi.
- (ii) Nywele zitunzwe na ziwe fupi. Ni marufuku kunyoa vipara au panki, kucaa nguo za kubana na kuonyesha maumbo ya mwili, kufuga ndevu na kucha ndefu, mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.
- (iii) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea vilabu nya pombe, na nyumba za kulala wageni.

## **2.5: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi
2. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyia
3. Uvutaji wa bangi
4. Makosa ya jinai.
5. Unyanyasaji wa kijinsia au kimadarasa
6. Kupigana au kupiga
7. kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha kupata mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa mimba.
12. Kutofanya mazoezi na mitihani ya shule bila sababu ya msingi.
13. Kutohudhuria shule kwa muda wa siku 90 mfululizo bila sababu ya msingi.
14. Kugoma, kuchochea au kutishia usalama wa watu au mali ya umma.
15. Kukataa adhabu halali kwa makusudi
16. Kutumia SIMU shulenii. (**Usije na simu shulenii**)

## **2.6 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

- A) i) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu maelezo ya mwanafunzi .  
ii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- B) Fomu ya mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.
- C) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.  
Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara atakaporipoti shulenii.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII  
MIHAYO MHOJA MASANGU  
MKUU WA SHULE**

## **KIAMBATANISHO ‘A’**

### **HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**

**SHULE YA MSINGI IMALA  
S.L.P 129  
URAMBO**

#### **i) HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi .....
2. Tarehe ya kuzaliwa..... utaifa.....
3. Jina la baba .....
4. Jina la mama .....
5. Jina la mlezi .....
6. Anuani kamili ya mzazi/mlezi .....
7. Uhusiano wa mlezi .....
8. Kazi ya mzazi/mlezi (mkulima/mfanyabiashara/ mfanyakazi) .....
9. Kama ni mfanya kazi kazi yake .....
10. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea .....
11. Kama mfanya biashara biashara yake ni .....
12. Afya yake (maelezo kama mwanafunzi anayo matatizo ya kiafya na hivyo anastahili  
huduma maalumu) .....
13. Michezo unayopendelea .....
14. Kama umewahi kuwa kiongozi, taja aina ya uongozi (shuleni).....
15. Madhehebu ya dini ya mwanafunzi .....

#### **ii) Uthibitisho wa mzazi/mlezi**

Mimi ..... Ninathibitisha kuwa maelezo yaliyotajwa hapo  
juu ni sahihi.

Na. ya simu ya mzazi/mlezi ..... Saini ..... Tarehe .....

## KIAMBATANISHO ‘B’

### **YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IMALA, NA KUTOSHIRIKI MIGOMO , FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi ..... ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kijiunga kidato cha kwanza Katika shule yako nimekubali binafsi kijiunga na shule hii. Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mtiifu, nitafuata sheria za shule na nitazingatia taratibu zote za shule, nitatunza mali zote za umma zilizopo hapo shulenii, nitasoma na kufanya kazi zote za shule kwa bidii na nitaishi kwa amani na kujiheshimu Katika Jumuiya ndani na nje ya shule. Hivyo kwa vyovoyote vile sitajihuisha kuanzisha wala kushiriki makosa ya migomo, fuj na makosa ya jinai na ikitokea nimeshiriki hatua kali za kinidhamu (kufukuzwa shule)zichukuliwe.

..... Tarehe.....  
Saini ya mwanafunzi

Mimi .....

Mzazi/mlezi wa ..... naahidi kutimiza wajibu ufuatao:-

1. Kuhakikisha kuwa mtoto wangu anafika shulenii kwa kuzingatia maagizo yaliyotolewa.
2. Kuhakikisha kuwa mtoto wangu awapo nyumbani ninampatia muda wa kutosha na mazingira mazuri kwa ajili ya kujifunza na kufanya mazoezi aliyopatiwa na walimu wake na nitamuelekeza pale inapowezekana.
3. Nitawajulisha walimu mara kwa mara mabadiliko mabaya Katika tabia ya mtoto wangu.
4. Nitatoa ushirikiano chanya Katika jitihada zote za kuboresha taaluma shulenii.

**NB: Ndugu wa karibu wa mwanafunzi.**

Jina	Mahusiano	Namba za simu
i.....	.....	.....
ii.....	.....	.....
iii.....	.....	.....
.....	.....	.....

**Jina na saini ya mzazi/mlezi**

**KIAMBATANISHO ‘C’**

**(To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster)**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**TO: THE MEDICAL OFFICER**

**FROM: .....**

.....  
.....

**DATE: .....**

**MR/MRS/MISS**

**(Name in full)**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for full time of his/her training course. (Form one to four). The examination should include the following categories.

- I a) Eye
- b) Hearing
- c) Limbs
- d) Speech
- e) Venereal Diseases
- f) Leprosy
- g) Epilepsy

**II NEUROSES**

**III Pregnancy**

**IV Other Serious Disease**

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE:**

**(To be completed a Government Medical Officer)**

I have examined the above named and consider that/she/he is physical fit/unfit and Mentally+ for a full time student training courses.

- I a) Eye sight .....
  - b) Hearing .....
  - c) Limbs .....
  - d) Speech .....
  - e) Venereal Diseases .....
  - f) Leprosy .....
  - g) Epilepsy .....
- II Neuroses .....
- III Pregnancy.....
- IV Other Serious Disease .....

**DATE: ..... SIGNATURE: .....**

**STATION: ..... DESIGNATION: .....**